بسم الله الرحمن الرحيم

FADHILA YA SUNNA ZA MTUME (S.A.W)

Imeandaliwa na: Abubakari Shabani Rukonkwa

Imepitiwa na: Yunus Kanuni Ngenda

Utangulizi:

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote, na rehma na amani zimwendee kiongozi wa umma huu Mtume wetu Muhammad (s.a.w) na watu wake na Maswahaba zake wote,! Amma baad.

Ni wazi kwamba Sunna za Mtume wetu Muhammad (s.a.w) ndio kielelezo na uhimili katika dini yetu ya kiislam, pia ndio tafsiri ya mwongozo mzima wa maisha ya mwislam kidini na kijamii kwa ujumla, hivyo mwislam hawezi kuwa na imani thabiti kama hajafuata sunna za Mtume Muhammad (s.a.w).

Hii inamaana kwamba yeyote aliye mbali na sunna basi yuko mbali na dini, na aliyekaribu na sunna yupo karibu na dini, Mwenyezi Mungu mtukufu anatilia mkazo na kuamrisha katika Qur’an pale alipo sema:

{وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَاب}

Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

[Surat Hashri: 7.

Ayah hii tukufu imekusanya sunna zote alizokuja nazo Mtume wetu Muhammad (s.a.w) ya kwamba hatuna budi kuzipokea na kuzifanyia kazi, ikiwa ni pamoja na kuzilinda, kuzinusuru na kuzieneza ulimwenguni kote.

Hili ni jambo kubwa lenye fadhila nyingi kwa yeyote mwenye kujishughulisha nalo, na ni sababu ya pata mwisho mwema na kuipata Jannah (Pepo).

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم:

Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake:

بدأ الإسلامُ غريبًا وسيعودُ غريبًا كما بدأ فطُوبِى للغرباءِ، وفي روايةٍ قيل يا رسولَ اللهِ : مَن الغرباءُ؟

Uislam ulianza ni mgeni na utarudi ni mgeni kama ulivyoanza, lakini habari njema ni kwa wale wanao onekana ni wageni (maghurabaa). (Pia inasemekana kwamba “TWUUBAA” ni mti katika miti ya peponi.

Na katika riwaya nyingine akaulizwa Mtume (s.a.w): Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni kina nani hao wanao onekana wageni (maghurabaa)? Akasema Mtume (s.a.w):

قال : الذين يصلحون إذا فسد الناسُ، وفي لفظٍ آخرَ قال : هم الذين يُصلِحون ما أفسد الناسُ من سنتي

Ni watu ambao wanatengeneza (palipo haribika) wanapoharibu watu (Dini).

Na katika lafdhi nyingine: Hao ni watu ambao wanatengeneza yaliyo haribiwa na watu kutokana na sunna zangu.

المصدر: مجموع فتاوى ابن باز الصفحة أو الرقم: ٣/١٥٨

خلاصة حكم المحدث: صحيح

Chanzo: Majumuu fatawa Ibun Baaz namba 3/158.

Na katika Hadithi nyengine.

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم :

كلُّ أمتي يدخلون الجنةَ إلا من أبى . قالوا : يا رسولَ اللهِ ، ومن يأبى ؟ قال : من أطاعني دخل الجنةَ ، ومن عصاني فقد أبى.

Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake: “Umati wangu wote wataingia Peponi isipokua atakae

kata”, wakasema (Maswahaba): Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni nani basi atake kata? Akasema: “Mwenye kunitii ataingia Peponi na mwenye kuniasi basi huyo amekataa.”

Ameipoke Imamu Bukhari, katika Hadhithi iliyotokana na Abuu Hurayra.

Kitabu ni: Swahihi Bukhari ukurasa namba 7280.

Hivyo shime ndugu zngu katika imani tushikamaneni na sunna za bwana Mtume Muhammad (s.a.w) hata kama jamii itakuona umekuja na mambo mageni, au hata ukipewa majina yasofaa hilo usijali bali hata Mtume (S.A.W) aliitwa mchawi a kaitwa mwendawazimu lakin aliendelea kuitangaza dini na kueneza Sunna zake (s.a.w).

Mfano ulio hai ni wanislam wanaoifanyia kazi kauli ya bwana Mtume (s.a.w) ya kupunguza nguo iliyozidi katika kongo mbili za miguu kwa wanaume utakuta baadhi ya watu wana watukana na kuwabeza kwa kuwapa majina yasiyofaa kama : njiwa, au kavaa nguo ya mtoto, au kavaa kimini sketi nk.

Hayo yakikukuta basi usikate tama unatakiwa kushikamana na sunna tu bila kujali matusi na kebehi za maadui wa haki.

Au kauli za baadhi ya watu kuwa eti huu sio wakati wa kuambiana kuhusu ndevu, kukata nguo inayozidi chini, na mfano wa hayo.

Hizi zote ni sauti za shari zinazokurudisha nyuma katika kufata maamrisho ya Mtume wetu Muhammad swallah llah alayhi wasalam.

Bali juwa kuwa ukifanya bidaa moja basi umeuwa suna iliyostahiki kuwa mahala hapo.

Na ukishika sunna basi juwa umefanya juhudi kubwa ya kuzuia bidaa.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu mshindi na mtukufu atudumishe katika Sunna za Mtume wetu Muhammad (s.a.w) na atukutanishe nae katika Pepo ya Firdausi, pamoja na wema waliokuja baada yake, Ameen!!.